

Matumizi mwafaka ya udongo jiko

- Tumia kuni katika miti yenye moshi ya chini.
- Tia jiko motoni hapo awali ili kuongeza joto ndani ya kijisanduku cha joto kisha utumie kijiti kimoja hadi viwili kupikia.
- Panga kupika vyakula zaidi ya kimoja kila mara ili kuhifadhi kuni.
- Funika chungu cha kupikia ili kupunguza masaa ya kupika.
- Tia chakula kinachopikwa ndani ya maji kabla ya kupika ili kupunguza muda wa kupika.



Kutumia jiko

Ulinzi wa kila mara

Kipande kimoja kikianguka kwa sababu ya kuathirika, kitoe kwa kutumia kisu. Mwangilia pahali palipo katika maji kisha uunganishe na udongo uliochanganywa vizuri.

Changamoto

Jiko lenyewe huzeeka na huitaji kutengenezwa kila mara.

Kuunda kunahitaji ujuzi kiasi zingatia: likifumwa vyema, jiko udongo huhifadhi hadi asilimia 30 ya kuni zinazotumika katika jiko la mawe la kiasili.



Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 5781 I, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Barua pepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

Mtayarishaji:

Adongo A.O.

Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

Mkuu wa Kituo

KARI-Marsabit, S.L.P. 147-60500

Simu: 069-2040/22220

Nukulishi: 069-2220

Vijitabu vya KARI vya taarifa nambari / 41 / 2008

Shilingi 20 za Kenya

Hifadhi kuni: Tumia jiko la udongo



Utangulizi

Jiko la udongo limetokana na kuimarishwa kwa jiko la kiafrika la kitamaduni ambalo lilikuwa na mawe matatu, manne au sita kulingana na jamii. Meko haya huundwa kwa kutumia udongo uliimarishwa na mawe kwenye kuta na kutiwa sanduku la moto kwenye kiini ili kuyafanya yawe imara. Jiko hili likitumiwa namna ya kuni inayofaa linaweza kuhifadhi asilimia 30 ya kuni. Manufaa mengine ni kuwa ni stadi unapopikia, hutoa moshi uliopungua, haichomi mifugo wachanga na hukipa chakula ladha nzuri.

Vifaa Vinavyohitajika

Mawe (aina ya quartz), udongo wa clay, majani, chembechembe za mawe madogo, maji, mwiko, jembe, panga na kisu.



Jinsi Ya Kuchanganya Udongo

Changanya mchanga wa clay au anthill, majivu na mavi ya ng'ombe katika vipimo vya 3:1:1 kabisa kwa kutumia mwiko au jembe. Ongeza maji kidogo kidogo huku ukichanganya hadi mchanga uwe tayari kuunda jiko.

Kuandaa mahali pa kuota moto

Pangilia jiko pembeni mwa nyumba kusikotumiwa na watu wengi.

- Acha nafasi kati ya jiko na ukuta, kisha uchonge mviringo wenye upana wa sentimita 68.
- Chimba mviringo huu undani wa sentimita 15.

- Jaza ulipochimba kwa vijawe.
- Jenga sehemu hii kwa udongo uliotayarisha.
- Dumisha sehemu ya nje kwa kugongelea na kifaa tambarare.
- Fanya sehemu zote ziwe nyororo kwa kutumia udongo kuunda jiko.

Kuunda jiko

1. Panga mawe kama ulivyoonyshwa hapa chini.



2. Kila unapotia udongo iliolowa, tia vijawe juu ili kujenga kuta za kudumu.



3. Endelea hadi mjengo ufkie kiwango cha kufunikia chungu.




4. Wekelea chungu kilichofinyangwa punde tu juu ya mawe kisha endelea kujengelea laini mbili hadi ufunike robo ya chungu.

5. Fungua njia ya moto ili chungu kiwe mahali pake.



6. Unapozungusha, toa chungu kisha ulainishe kando kufunguliwa kwa juu.



7. Unda mahali pa chungu kukalia na utoe inchi kadhaa kwenye pande ya juu ili kuhakikisha hewa inaingia na kupunguza kutoka kwa moshi.



Kufunikia

- Funika mahali kokote kulio na nyufa ukitumia mavi ya ng'ombe yaliyo changanywa na majivu. Endelea kufanya hivi hadi kuvujika kusikuwepo.

Ikisha kauka kabisa, washa moto ndani na uwache uchome kwa muda wa nusu saa hadi vifaa vyote kutoka kwenye ardhi vimechomeka na moshi umeisha.